# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

***(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)***

**Sehemu ya CXXXIV Nam. 7352** **13 Juni, 2025** **Bei Shs.8,000/=**

*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti* *Hutolewa kila Ijumaa*

**YALIYOMO** **UK**

Sheria ya Huduma Ndogo Ndogo za Fedha Zanzibar Nam.9 ya 2023
Kanuni za Huduma Ndogo Ndogo za Fedha Zanzibar (Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo ) ........................................................................ 799

**SEHEMU YA SHERIA**

Sheria iliyotajwa hapo chini imetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

**Tangazo la Sheria**

Nam. 58:- Kanuni za Huduma Ndogo Ndogo za Fedha Zanzibar (Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo ) .

## SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA ZANZIBAR, NAM. 9 YA 2023

## KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA ZANZIBAR (VYAMA VYA USHIRIKA VYA AKIBA NA MIKOPO)

**[Chini ya kifungu cha 61(1)]**

### MPANGILIO WA KANUNI

**KANUNI** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.

**Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjikia kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakla zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.**

**SEHEMU YA PILI**
**UTARATIBU WA UTOAJI WA LESENI**

4. Maombi ya leseni.
5. Katazo la kutoa huduma ndogo za fedha bila ya leseni.
6. Mazingatio ya maombi.
7. Kukataa kutoa leseni.
8. Ukaguzi kabla ya kutoa leseni.
9. Uhalali wa leseni
10. Upandishaji daraja wa leseni ya SACCOS.
11. Kufutwa kwa leseni.
12. Shughuli zinazoruhusiwa.
13. Shughuli zisizoruhusiwa.
14. Sehemu ya biashara.
15. Kufungua matawi.
16. Kuhamisha sehemu ya biashara.
17. Kuendesha kituo cha huduma.

**SEHEMU YA TATU**
**UTOSHELEVU WA MTAJI**

18. Kiwango cha chini cha mtaji.
19. Katazo la kuhamisha mtaji.
20. Mfuko wa akiba ya lazima.
21. Mgawanyo wa faida halisi.
22. Malipo ya gawio, faida na migao mengine.
23. Mpango wa kuongeza mtaji.

**SEHEMU YA NNE**
**UTAWALA**

24. Kamati ya uongozi.
25. Kazi ya kamati ya uongozi.
26. Uchunguzi na kuwaondolea sifa wajumbe wa kamati ya uongozi.
27. Uteuzi na kazi za kamati ya mikopo.
28. Ajira na majukumu ya meneja wa SACCOS.

**SEHEMU YA TANO**
**SHUGHULI ZA UKOPESHAJI**

29. Sera ya mikopo.
30. Maombi ya mikopo.
31. Uidhinishaji wa mkopo.
32. Mkataba wa mkopo.
33. Sababu za kukataliwa mkopo.
34. Dhamana ya mkopo.
35. Udhamini wa mkopo.
36. Miamala ya watu wanaohusiana.
37. Urejeshaji wa mkopo kabla ya muda.

38. Vigezo na masharti ya mikopo shirikishi.
39. Mikopo iliyocheleweshwa kulipwa.
40. Makundi na tengo la mikopo.
41. Limbikizo la tozo kwa mikopo iliyocheleweshwa kulipwa.
42. Kukusanya au kufuatilia mikopo.
43. Ufutaji wa deni.

**SEHEMU YA SITA**
**USIMAMIZI WA UKWASI, MALI NA DHIMA**

44. Sera ya usimamizi wa mali na dhima.
45. Mpango wa dharura wa ukwasi.
46. Kiwango cha chini cha uwiano wa ukwasi wa mali.
47. Amana katika benki.
48. Ukopaji nje ya SACCOS.
49. Sera ya uwekezaji.
50. Masharti ya uwekezaji.

**SEHEMU YA SABA**
**HESABU NA UKAGUZI**

51. Vitabu vya hesabu na kumbukumbu.
52. Mwaka wa fedha.
53. Uandaaji na uwasilishaji wa hesabu.
54. Uoneshaji wa taarifa za fedha.
55. Mkaguzi wa ndani.
56. Taarifa ya mkaguzi wa ndani.
57. Majukumu ya mkaguzi wa ndani.
58. Mpango wa ukaguzi wa ndani.
59. Ukaguzi wa nje.
60. Mkaguzi wa nje kuwasiliana na waajiriwa.
61. Kutoa taarifa za ukiukwaji.
62. Kuwasilisha taarifa za ukaguzi katika Mkutano Mkuu wa Mwaka.
63. Kubadilisha mkaguzi wa nje.

**SEHEMU YA NANE**
**USIMAMIZI NA UKAGUZI**

64. Ukaguzi wa SACCOS.
65. Uwasilishaji wa taarifa za vipindi.
66. Makubaliano ya usimamizi.
67. Utoaji wa amri ya zuio na katazo.
68. Usimamizi na uchukuaji.
69. Ukomo wa usimamizi wa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

**SEHEMU YA TISA**
**KUMLINDA MLAJI**

70. Masharti ya uwazi wa hisa, akiba na amana.

71. Mfumo wa utatuzi wa malalamiko na migogoro.
72. Elimu ya fedha.

**SEHEMU YA KUMI**
**MASHARTI MENGINEYO**

73. Mpango wa mwendelezo wa biashara.
74. Uwasilishaji wa taarifa za mikopo.
75. Ridhaa ya kubadilishana taarifa za mikopo.
76. Hatua za kiutawala.
77. Rufaa.
78. Kipindi cha mpito.
79. Makubaliano kati ya SACCOS na mwajiri.

MAJADWELI

## SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA ZANZIBAR, NAM. 9 YA 2023

## KANUNI ZA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA ZANZIBAR (VYAMA VYA USHIRIKA VYA AKIBA NA MIKOPO)

**[Chini ya Kifungu 61(1)]**

**KWA UWEZO** niliopewa chini ya kifungu cha 61(1) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar, Nam. 9 ya 2023, **Mimi, DKT. SAADA MKUYA SALUM,** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, natunga Kanuni zifuatazo:

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar (Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo), 2025 na zitaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Waziri na kutangazwa katika Gazeti Rasmi.

Matumizi.

**2.** Kanuni hizi zitatumika kwa watoa huduma ndogo za fedha wote walio katika Daraja la Tatu wanaotoa huduma Zanzibar.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"amri ya zuio na katazo" "maana yake ni amri ya kiutawala inayochukuliwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa dhidi ya SACCOS ili kuzuia mambo yasiyo salama na yasiyo na tija yasitokee;

"Benki" ina maana kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Nam. 4 ya 2006;

"Chombo cha Ubadilishanaji wa Taarifa za Mikopo" ina maana kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria;

"Daraja la Tatu" maana yake ni watoa huduma wa huduma ndogo za fedha wanaohusika na Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo;

"hisa za hiari" maana yake ni fedha ambazo zinawekwa na mwanachama na zinaweza kutumika kama dhamana kwa mujibu wa vigezo na masharti yaliyoainishwa katika sheria za SACCOS;

"Idara" maana yake ni Idara ya Maendeleo ya Ushirika iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar, Nam. 15 ya 2018;

"karadha ndogo" maana yake ni shughuli za karadha ya fedha ambapo wastani wa thamani ya orodha ya mali inafikia shilingi milioni kumi na muda wa ukomo wa karadha hiyo hauzidi miezi ishirini na nne;

"kituo cha huduma" maana yake ni sehemu ya biashara ya SACCOS ambayo sio tawi lililoidhinishwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kuendesha shughuli za SACCOS;

"Mamlaka Iliyokasimiwa" maana yake ni Idara ya Maendeleo ya Ushirika iliyokasimiwa na Benki kutekeleza kazi na uwezo wa Benki kuhusiana na Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo kwa mujibu wa Sheria;

"mtaji halisi" maana yake ni hisa za wanachama zilizolipwa kwa ukamilifu, mfuko wa akiba za lazima, limbikizo la ziada, misaada kwa ajili ya mtaji na michango ambayo haihamishiki na ambayo haikusudiwi kurejeshwa isipokuwa kama SACCOS imewekwa kwenye ufilisi;

"mtaji wa taasisi" maana yake ni malimbukizi ya faida, misaada na michango ambayo haikusudiwi kutumika isipokuwa pale ambapo SACCOS imewekwa kwenye ufilisi;

"mtumiaji" maana yake ni mteja au mwanachama wa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha ambaye anapata au anakusudia kupata huduma kutoka kwa mtoa huduma wa huduma ndogo za fedha;

"SACCOS" maana yake ni Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya Zanzibar, Nam.15 ya 2018;

"sehemu ya biashara" maana yake ni tawi, ofisi, wakala, kituo cha huduma au huduma inayohama ya SACCOS iliyowazi kwa umma;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar, Nam. 9 ya 2023;

"taarifa ya mkopo" maana yake ni taarifa yoyote inayohusiana na utambulisho mahsusi wa mkopaji, jina kamili, tarehe ya kuzaliwa, sehemu ya makaazi, sehemu ya makaazi ya awali, hali ya ndoa, jina la mwenza, sehemu ya ajira, sehemu ya awali ya ajira, tabia ya ulipaji, dhima ya deni liliopo, mali na uchunguzi uliofanyika wa historia ya mkopo au taarifa inayohusiana na taasisi za kisheria au biashara ambayo ingeweza kuitambua au taarifa ya biashara inayohusiana na usajili, kodi, wakurugenzi, usimamizi, na taarifa nyengine za biashara;

"tawi" maana yake ni sehemu ya biashara ya SACCOS tofauti na sehemu yake ya ofisi kuu, ambayo imeidhinishwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kujiendesha kiutawala kama tawi;

"tozo" inajumuisha riba, faida, gharama na malipo, ada za uchakataji wa mkopo na malipo mengine;

"Ukwasi'' maana yake ni uwezo wa SACCOS kubadilisha mali zake kuwa fedha taslimu au kupata fedha taslimu ili kulipa au kutimiza majukumu yake ya muda mfupi;

"uwakala wa benki" maana yake ni biashara ya kutoa huduma za kibenki kwa niaba ya taasisi ya kibenki chini ya mkataba halali wa uwakala; na

"Waziri" ina maana kama ilivyotafsiriwa chini ya Sheria.

## SEHEMU YA PILI
## UTARATIBU WA UTOAJI WA LESENI

Maombi ya leseni.

**4.-**(1) Kwa kuzingatia kifungu cha 18(2) cha Sheria, SACCOS inayokusudia kutoa huduma ndogo za fedha itaomba leseni Benki au kwa Mamlaka Iliyokasimiwa kwa kujaza fomu ya maombi ya leseni iliyoainishwa chini ya Jadweli la Kwanza la Kanuni hizi.

(2) Muombaji wa leseni atalipa ada isiyorejesheka ya:

(a) Shilingi Laki Tatu kwa Leseni ya Daraja A; na

(b) Shilingi Laki Moja na Elfu Hamsini kwa Leseni ya Daraja B.

(3) Maombi yaliyotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii yatasainiwa na muombaji au mwakilishi aliyeidhinishwa na muombaji na yataambatanishwa na:

(a) nyaraka na taarifa zilizoorodheshwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi; na

(b) nyaraka nyengine au taarifa yoyote kama itakavyohitajika.

Katazo la kutoa huduma ndogo za fedha bila leseni.

**5.-**(1) SACCOS haitatoa huduma ndogo za fedha zozote ya kupewa leseni na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria.

(2) SACCOS yoyote itakayokiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii itakuwa imetenda kosa, na ikitiwa hatiani itapewa adhabu iliyoainishwa chini ya kifungu cha 6 (2)(b) cha Sheria.

Mazingatio ya maombi.

**6.-**(1) Kwa kuzingatia kanuni ya 4 ya Kanuni hizi, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, ndani ya siku thelathini kutoka tarehe ya kupokea maombi yaliyokamilika, itayakubali au kuyakataa maombi hayo.

(2) Endapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa imepokea nyaraka za maombi ya leseni ambazo hazijakamilika, kabla ya kushughulikia maombi hayo, itamtaka muombaji:

(a) kuwasilisha nyaraka au taarifa zinazokosekana au nyaraka za nyongeza; au

(b) kusahihisha au kurekebisha mapungufu yanayohusiana na masharti ya utoaji wa leseni.

(3) Endapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa imekubali maombi, itatoa leseni kama ilivyoainishwa chini ya Jadweli la Tatu la Kanuni hizi.

Kukataa kutoa leseni.

**7.-**(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kukataa kutoa leseni endapo:

(a) muombaji ameshindwa kukidhi vigezo na masharti yaliyoainishwa kwa ajili ya kupewa leseni; au

(b) muombaji ametoa taarifa za uongo au zinazopotosha.

(2) Endapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa imekataa kutoa leseni, itamjulisha muombaji kwa maandishi sababu za kukataa kutoa leseni ndani ya siku saba tokea tarehe ya uamuzi huo.

(3) Muombaji ambaye maombi yake yamekataliwa anaweza kuomba tena, iwapo amesahihisha mapungufu yaliyosababisha maombi ya awali kukataliwa.

Ukaguzi kabla ya kutoa

**8.** Kabla ya kutoa leseni, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kufanya ukaguzi wa eneo la biashara, miundo mbinu ya mawasiliano, mifumo ya uhasibu na udhibiti wa ndani wa SACCOS.

Uhalali wa Leseni.

**9.-**(1) Leseni iliyotolewa chini ya Kanuni hizi itaendelea kuwa halali isipokua kama itasitishwa au kufutwa kwa utaratibu ulioainishwa katika Sheria.

(2) Leseni iliyotolewa chini ya Kanuni hizi itafikia ukomo wake iwapo biashara haitaanza kutoa huduma ndani ya miezi sita tangu tarehe ya kutolewa kwa leseni.

Upandishaji daraja wa leseni ya SACCOS.

**10.** Endapo SACCOS yenye leseni ya daraja B, imekidhi masharti ya mtaji wa leseni ya daraja A, inaweza kuomba leseni ya daraja A.

Kufutwa kwa leseni.

**11.-**(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza, kwa kutoa notisi kwa SACCOS, kufuta leseni endapo SACCOS:

(a) imeacha kutoa huduma ndogo za fedha ndani ya mwaka mmoja;

(b) imekiuka masharti na vigezo vilivyoainishwa kwenye

leseni;

(c) imefilisiwa au imeshindwa kujiendesha;

(d) imefutiwa usajili kwa mujibu wa sheria husika ; au

(e) imekiuka masharti ya Sheria.

(2) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itasababisha jina la SACCOS ambayo leseni yake imefutwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali na kwenye gazeti linalowafikia watu wengi ndani ya siku kumi na nne tokea kufutwa kwa leseni hiyo.

Shughuli zinazo-ru-husiwa.

**12.-**(1) SACCOS yenye leseni daraja A inaweza kufanya shughuli zifuatazo:

(a) Shughuli zote zilizotajwa katika kanuni ndogo ya (2);

(b) karadha ndogo;

(c) kupokea amana kutoka kwa wanachama wake;

(d) kushiriki katika mikopo shirikishi;

(e) wakala wa bima;

(f) wakala wa huduma za kibenki;

(g) wakala wa mitandao ya simu

(h) kufanya uwekezaji katika hisa, hati fungani au miradi ya kiuchumi; na

(i) kutoa kadi za malipo ( Credit cards, prepaid cards ).

(2) SACCOS yenye leseni daraja B inaweza kufanya shughuli zozote kati ya zifuatazo:

(a) kupokea hisa za uanachama na hisa za hiari;

(b) kupokea akiba kutoka kwa wanachama;

(c) kutoa mikopo kwa wanachama wake;

(d) kufanya uwekezaji;

(e) wakala wa huduma za kibenki; na

(f) wakala wa mitandao ya simu.

Shughuli zisizo-ru-husiwa.

**13.** SACCOS hairuhusiwi kujihusisha na shughuli yoyote kati ya zifuatazo:

(a) kufungua akaunti ya fedha za kigeni kwa wateja wake;

(b) kupokea amana kutoka kwa watu wasio wanachama wake;

(c) kufanya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni;

(d) kufanya biashara za kimataifa;

(e) shughuli za udhamini;

(f) katoa kadi za malipo (Debit Cards); na

(g) kuhamisha fedha na kutoa amri za malipo.

Sehemu ya biashara.

**14.** Kila SACCOS itakuwa na:

(a) sehemu au eneo la biashara lenye anuani sahihi kwa ajili ya kutoa

(b) huduma ndogo za fedha; na

(c) kuonesha kwa uwazi jina lake la biashara katika sehemu ya biashara.

Kufungua matawi.

**15.-**(1) SACCOS yenye leseni ya daraja A inayotaka kufungua tawi ili kuongeza wigo wa shughuli zake, itaomba idhini kwa maandishi kutoka Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

(2) Maombi yalioletwa chini ya kanuni ndogo ya (1) yataambatishwa na yafuatayo:

(a) eneo linalopendekezwa kwa ajili ya kufungua tawi;

(b) lengo na madhumuni ya kufungua tawi jipya;

(c) bajeti iliyochanganuliwa na chanzo cha fedha za uanzishaji wa tawi hilo;

(d) makisio ya mizania na taarifa ya mapato na matumizi kwa muda wa miaka miwili baada ya tawi kuanza shughuli zake;

(e) mapendekezo ya muundo wa tawi, majina na wasifu binafsi wa mkuu wa tawi; na

(f) taarifa nyingine yoyote kama Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itakavyohitaji.

(3) Katika kutathimini maombi chini ya kanuni ndogo ya (2), Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itazingatia yafuatayo:

(a) uwezo wa kujiendesha wa tawi linalopendekezwa:

(b) uwezo wa kifedha wa SACCOS kuendesha tawi linalopendekezwa;

(c) endapo SACCOS inakidhi kiwango cha chini cha mtaji unaohitajika;

(d) weledi na uwezo wa watendaji wa tawi linalopendekezwa;

(e) endapo tawi linalopendekezwa linakidhi vigezo vya usalama angalau kwa kiwango cha chini kama itakavyoelekezwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa; na

(f) kigezo chengine chochote kadiri itakavyoelekezwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

(4) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kufanya ukaguzi wa jengo la tawi linalopendekezwa kabla ya kuanza uendeshaji.

(5) SACCOS yenye leseni daraja B haitaruhusiwa kufungua tawi.

**16.** SACCOS ambayo inakusudia kuhamisha sehemu yake ya biashara itaomba idhini kwa maandishi kutoka kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa na maombi hayo yataambatishwa na taarifa zifuatazo: Kuhamisha sehemu ya biashara.

(a) sababu za kuhamisha;

(b) anuani halisi ya sehemu mpya ya kutoa huduma; na

(c) taarifa nyengine yoyote kama Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itakavyohitaji.

**17.-**(1) SACCOS haitafungua au kuendesha kituo cha huduma bila ya idhini ya maandishi ya Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa iliyotolewa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi. Kuendesha kituo cha huduma.

(2) Ombi la idhini lililotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1) litaambatanishwa na yafuatayo:

(a) taarifa ya hali ya usalama na nafasi iliyopo kwa ajili ya SACCOS kutoa huduma na bidhaa za mikopo; na

(b) taarifa nyengine yoyote kama Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itakavyohitaji.

## SEHEMU YA TATU
## UTOSHELEVU WA MTAJI

**18.-**(1) SACCOS yenye leseni daraja A itaanza kutoa huduma na kuhakikisha muda wote ina mtaji usiopungua shilingi za kitanzania milioni mia moja. Kiwango cha chini cha mtaji.

(2) SACCOS yenye leseni daraja B itaanza kutoa huduma na kuhakikisha muda wote ina mtaji usiopungua shilingi za kitanzania milioni tano.

(3) Kila SACCOS itatakiwa muda wote kuwa na:

(a) mtaji halisi usiopungua asilimia nane ya jumla ya mali zote;

(b) mtaji wa taasisi usiopungua asilimia sita ya jumla ya mali zote; na

(c) mtaji kamili wa taasisi usiopungua asilimia sita ya jumla ya mali zote.

Katazo la kuhamisha mtaji.

**19.** Isipokuwa kama imeidhinishwa vyenginevyo na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, SACCOS haitahamisha fedha kutoka kwenye mtaji halisi au mfuko wa akiba ya lazima endapo uwiano wa mtaji wa taasisi ni pungufu ya uwiano wa chini unaohitajika.

Mfuko wa akiba ya lazima.

**20.** Kila SACCOS itaanzisha mfuko wa akiba ya lazima na mtaji wa taasisi kwa kuzuia angalau asilimia thelathini na tano ya faida halisi baada ya matumizi na gharama zote kulipwa.

Mgawanyo wa faida halisi.

**21.** Kwa kuzingatia kanuni ya 20 ya Kanuni hizi na sheria ndogo za SACCOS, SACCOS inaweza kugawa kiasi chochote kilichosalia cha faida halisi baada ya gharama zote kulipwa na masharti ya mtaji kufikiwa kwa ajili ya madhumuni yafuatayo:

(a) gawio la hisa;

(b) tengo kwa ajili ya mfuko wa maendeleo au mfuko mwengine utakavyoamuliwa na SACCOS na

(c) mchango kwa ajili ya hisani, elimu, matibabu au malengo mengine kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika;

(d) malipo mengine kama yatakavyoidhinishwa na mkutano mkuu wa mwaka.

Malipo ya gawio, faida na migao mengine.

**22.-**(1) Kwa kuzingatia kifungu cha 33 cha Sheria, kila SACCOS itaeleza katika kanuni zake utaratibu wa malipo ya lazima ya gawio, hisa au aina yoyote ya mgao kwa wanachama wake ikijumuisha namna na kipindi ambacho malipo hayo yatafanyika.

(2) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), malipo ya gawio au aina yoyote ya mgao hayatafanyika kutoka katika faida halisi isipokuwa kama:

(a) Mtaji wa taasisi na mtaji halisi wa taasisi ikilinganishwa na uwiano wa jumla wa mali unafikia sharti la kiwango cha chini kilichowekwa;

(b) kiasi cha akiba ya lazima kinatosha kufidia limbikizo la hasara la SACCOS;

(c) kiasi cha akiba ya lazima, tengo la mikopo isiyolipika na mfuko wa kukombolea hisa vimetengwa; na

(d) baada ya kupata ridhaa ya mkutano mkuu.

Mpango wa kuongeza mtaji.

**23.-**(1) Endapo SACCOS imeshindwa kufikia masharti ya kiwango cha chini cha mtaji kama ilivyoelekezwa katika Kanuni hizi, SACCOS hiyo itatakiwa ndani ya siku sitini za mapungufu hayo, kuwasilisha Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa mpango wa kuongeza mtaji wake.

(2) Mpango wa kuongeza mtaji ulioainishwa chini ya kanuni ndogo ya (1), kwa uchache, utaeleza yafuatayo:

(a) hatua zitakazochukuliwa na uongozi ili mtaji kurudi katika kiwango cha chini kinachohitajika;

(b) muda unaohitajika ili mtaji kurudi katika kiwango cha chini kinachohitajika;

(c) kiwango cha mtaji kinacholengwa kufikiwa kila mwishoni mwa robo mwaka; na

(d) taarifa nyengine yoyote kama Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itakavyohitaji.

(3) Endapo SACCOS imeshindwa kufikia kiwango cha chini cha mtaji na imeshindwa kuwasilisha au kutekeleza mpango wa kuongeza mtaji, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kuchukua hatua za usimamizi kama itakavyoona inafaa.

## SEHEMU YA NNE
## UTAWALA

**24.-**(1) Kila SACCOS itakuwa na kamati ya uongozi inayoundwa na watu wasiopungua saba na wasiozidi tisa waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa SACCOS. Kamati ya uongozi.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), mtu atakuwa na sifa za kuwa mjumbe wa kamati ya uongozi ikiwa:

(a) ana uwezo wa kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili;

(b) ana uadilifu wa kiwango cha juu;

(c) sio kiongozi wa SACCOS nyengine; na

(d) masharti mengine kama yalivyoainishwa katika sheria ndogo za SACCOS.

**25.** Kamati ya uongozi ya SACCOS itatekeleza kazi zifuatazo: Kazi za kamati ya uongozi.

(a) kuhakikisha kuwa SACCOS inafanya shughuli zake kwa ufanisi na inazingatia masharti ya Sheria, Kanuni hizi, sheria ndogo za SACCOS na sheria nyengine yoyote inayohusika;

(b) kusimamia utekelezaji wa maazimio ya mkutano mkuu;

(c) kutunga sera sahihi kwa ajili ya mikopo, usimamizi wa ukwasi na mali, rasilimali watu, uwekezaji, akiba, fedha, utunzaji taarifa, na sera nyengine kama itakavyoamua;

(d) kuandaa mapendekezo ya SACCOS kukopa;

(e) kuhakikisha kuwa hesabu za SACCOS zinaandaliwa na kukaguliwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni hizi na sheria ndogo za SACCOS;

(f) kupendekeza malipo ya gawio kwa ajili ya kuidhinishwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kabla ya kuwasilishwa kwenye mkutano mkuu wa mwaka;

(g) kuandaa mpango endelevu na uokozi wa majanga na kuhakikisha mipango hiyo inajaribiwa mara kwa mara;

(h) kupitia bajeti ya mwaka ya SACOSS na kutoa mapendekezo kwa mkutano mkuu kwa ajili ya kupata idhini;

(i) kuidhinisha ajira za watumishi mahiri watakaosimamia shughuli za SACCOS; na

(j) kusimamia ufunguaji na matumizi ya akaunti za benki za SACCOS.

Uchunguzi na kuwaondolea sifa wajumbe wa kamati ya uongozi.

**26.-**(1) SACCOS haitafanya shughuli zake hadi pale wajumbe wa Kamati ya Uongozi watakapokuwa wamefanyiwa uchunguzi na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

(2) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kumwondolea sifa mjumbe wa Kamati ya Uongozi ya SACCOS endapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa imebaini kwamba mjumbe huyo:

(a) hana sifa zinazohitajika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi;

(b) amejihusisha na shughuli za kukosa uaminifu au udanganyifu;

(c) ana mikopo au madeni mengine yaliyocheleweshwa kwa zaidi ya siku tisini;

(d) amekutwa na mgongano wa maslahi utakaoathiri uhuru wake katika kutekeleza majukumu yake;

(e) amewahi kuhusika katika uendeshaji usiofaa wa SACCOS au taasisi yoyote ya fedha; na

(f) amevunja masharti yoyote ya Sheria husika.

(3) Endapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa imemwondolea sifa mjumbe wa Kamati ya Uongozi, mjumbe huyo atasita kujihusisha na shughuli za Kamati ya Uongozi.

Uteuzi na kazi za kamati ya mikopo.

**27.-**(1) Kila SACCOS itateua kamati ya mikopo kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa shughuli zake kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi na sheria ndogo za SACCOS.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), kamati ya mikopo itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kusimamia ufanisi wa utekelezaji wa sera ya mikopo;

(b) kuidhinisha maombi ya mikopo kwa mujibu wa vigezo na masharti yaliyowekwa na sera ya mikopo ya SACCOS husika;

(c) kusimamia marejesho ya mikopo kulingana na jadweli la marejesho;

(d) kupokea taarifa za mwenendo wa mikopo, ikijumuisha idadi, thamani na muda wa mikopo kutoka kwa meneja wa mikopo na kushauri ipasavyo;

(e) kuwasilisha taarifa za shughuli zake kwa kila kipindi husika kwa Kamati ya Uongozi kwa ajili ya kuzingatiwa na kupelekwa kwenye mkutano mkuu wa mwaka;

(f) kuomba ushauri na kupokea miongozo kutoka Kamati ya Uongozi kwa maombi ya mikopo yanayohitaji idhini maalumu; na

(g) kutekeleza majukumu mengine kwa mujibu wa Sheria, Kanuni hizi na sheria ndogo za SACCOS.

Ajira na majukumu ya meneja wa SACCOS.

**28.-**(1) SACCOS inaweza kuajiri mtu mwenye sifa ambaye atakuwa meneja wa SACCOS.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mtu aliyeajiriwa katika nafasi ya meneja pamoja na majukumu yaliainishwa katika sheria ndogo za SACCOS atatekeleza majukumu yafuatayo:

(a) kuhakikisha mifumo ya uendeshaji na utoaji wa taarifa ina ufanisi, uhakika na kurahisisha mawasiliano;

(b) kuandaa bajeti ya mwaka na mpango wa biashara kwa kushauriana na wajumbe wa Kamati ya Uongozi;

(c) kusimamia masuala yote ya watumishi ikiwemo maendeleo ya rasilimali watu na mafunzo;

(d) kuandaa na kutunza taarifa sahihi za fedha kwa wakati;

(e) kuwasilisha taarifa za uendeshaji katika mikutano ya Kamati ya Uongozi;

(f) kuidhinisha matumizi kulingana na bajeti iliyopitishwa na Kamati ya Uongozi;

(g) kuandaa na kuwasilisha taarifa za usimamizi kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kwa wakati;

(h) kutekeleza mapendekezo yaliyomo katika taarifa za ukaguzi wa nje, ukaguzi wa ndani na taarifa za usimamizi;

(i) kuhakikisha matakwa ya Sheria, kanuni, sera, sheria ndogo za SACCOS, taratibu na kanuni za maadili zinazingatiwa; na

(j) kutekeleza majukumu mengine kama itakavyoelekezwa na kamati ya uongozi.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) na (2), mtu atakayeajiriwa katika nafasi ya meneja wa SACCOS atatakiwa kuwa na:

(a) angalau diploma ya masuala ya fedha, uhasibu, utawala au fani nyengine inayohusiana na hizo, kwa SACCOS yenye leseni ya Daraja A; na

(b) uwezo wa kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili, kuhesabu na awe na uwezo wa kuendesha SACCOS yenye leseni ya daraja B.

(4) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, SACCOS inaweza kuajiri maafisa wengine ikijumuisha mhasibu, afisa mikopo, afisa mafunzo na afisa mwengine yeyote kadri itakavyohitajika kwa utekelezaji bora wa shughuli zake.

## SEHEMU YA TANO
## SHUGHULI ZA UKOPESHAJI

Sera ya mikopo.

**29.-**(1) Kila SACCOS itakuwa na sera ya mikopo inayoendana na masharti ya Sheria na Kanuni hizi.

(2) Sera iliyotajwa katika kanuni ndogo ya (1) itajumuisha yafuatayo:

(a) taratibu za ukopeshaji na nyaraka zinazohusika;

(b) masharti ya kukidhi kupata mkopo;

(c) aina za mikopo na dhamana zinazokubalika;

(d) ukomo wa mikopo ikijumuisha kiwango cha juu cha mkopo kwa mkopaji na kwa bidhaa ya mkopo;

(e) vigezo na masharti ya mkopo kama viwango vya faida, ada, tozo, idadi na muda wa marejesho;

(f) adhabu au ada kwa marejesho yaliyocheleweshwa;

(g) ukomo wa mkopo ukilinganishwa na thamani ya dhamana;

(h) masharti ya udhamini, pale inapohitajika;

(i) ufuatiliaji na tathimini ya ubora wa mikopo;

(j) kipindi kinachotolewa kabla ya kuanza kurejesha mkopo, kama kipo;

(k) utaratibu wa ukusanyaji na ufuatiliaji wa mikopo;

(l) vigezo na taratibu za kubadilisha masharti ya mkopo;

(m) vigezo na taratibu za kufuta mikopo iliyocheleweshwa kwa zaidi ya siku tisini;

(n) kipindi cha mkopo;

(o) fomu husika zinazotumika kwa ajili ya maombi ya mkopo; na

(p) taarifa nyengine yoyote muhimu kama itakavyoonekana inafaa kwa SACCOS.

**30.-**(1) SACCOS itahakikisha kuwa kila mwanachama anayekusudia kupata mkopo atawalisisha SACCOS fomu za maombi ya mikopo kwa kutumia fomu maalumu. Maombi ya mikopo.

(2) Fomu maalumu iliyotajwa katika kanuni ndogo ya (1) itajumuisha taarifa zifuatazo:

(a) jina kamili la muombaji;

(b) tarehe ya kuzaliwa au tarehe ya kusajiliwa;

(c) sehemu ya makazi, sehemu ya biashara au mahali pa kazi;

(d) taarifa za mawasiliano ikijumuisha namba za simu, anwani ya barua pepe na posta kama zipo;

(e) kazi au aina ya biashara;

(f) madhumuni ya mkopo;

(g) sekta ya uchumi;

(h) kiasi cha mkopo unaoombwa;

(i) dhamana iliyowekwa;

(j) hali ya ndoa;

(k) idadi ya wategemezi;

(l) kipato cha sasa;

(m) matumizi;

(n) mikopo mengine iliyopo; na

(o) taarifa nyengine kadri itakavyohitajika.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (2), fomu ya maombi ya mkopo itajumuisha sharti kwamba muombaji atatoa ridhaa na tamko kwamba taarifa zake za mikopo zinaweza kutolewa kulingana na masharti ya Sheria na Kanuni hizi.

**31.-**(1) SACCOS haitatoa mkopo bila kuidhinishwa na kamati ya mikopo. Uidhinishaji wa mkopo.

(2) Kamati ya mikopo haitaidhinisha mkopo isipokuwa kama mkopo wote au sehemu ya mkopo huo umedhaminiwa.

Mkataba wa mkopo.

**32.-**(1) SACCOS itashughulikia maombi ya mikopo kwa mujibu wa sera yake ya mikopo na iwapo itajiridhisha kuwa mkopaji amekidhi masharti ya mkopo na ana uwezo wa kulipa mkopo, itaingia katika mkataba wa mkopo na mkopaji.

(2) Mkataba wa mkopo uliotajwa katika kanuni ndogo ya (1) utaandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza kulingana na mahitaji ya mkopaji na utajumuisha yafuatayo:

(a) kiasi cha mkopo;

(b) ada na tozo zote;

(c) jadweli la marejesho ya mkopo linalojumuisha idadi ya marejesho, kiasi cha rejesho kwa kuainisha mkopo, tozo, ada na tarehe ya rejesho;

(d) jumla ya malipo yote hadi mwisho wa mkopo;

(e) adhabu kwa kuchelewesha marejesho;

(f) taratibu za kudai mkopo;

(g) notisi ya maslahi kwenye dhamana iliyotumika kudhamini mkopo, kama ipo

(h) saini ya mkopaji na afisa aliyeidhishwa na SACCOS;

(i) akiba au hisa zinazohitajika na endapo fedha hizo zinaweza kutumika kulipa deni la mkopo; na

(j) taarifa nyengine yoyote kama itakavyoelekezwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

Sababu za kukataliwa mkopo.

**33.** Endapo maombi ya mkopo yatakataliwa, SACCOS, ndani ya siku saba itamjulisha muombaji sababu za kukataliwa maombi yake.

Dhamana ya mkopo

**34.-**(1) Mkopo au jumla ya mikopo kwa mwanachama haitakiwi kuzidi asilimia kumi ya mtaji wa SACCOS isipokuwa kama mkopo huo umedhaminiwa kikamilifu kwa hisa za hiari, akiba, amana au mali.

(2) Endapo mkopo haujadhaminiwa kikamilifu kwa hisa za hiari, akiba, amana au mali, mkopo hautazidi asilimia tano ya mtaji wa SACCOS.

(3) Kabla ya kutoa mkopo, SACCOS itahakikisha kuwa:

(a) dhamana ya mkopo imeandikwa na kusajiliwa ipasavyo;

(b) mkopaji atatakiwa kuwa na idhini ya kisheria inayomruhusu kutumia dhamana husika iwapo mkopaji anatumia dhamana ya mtu mwengine;

(c) taarifa zote muhimu kuhusu dhamana husika zimeingizwa katika daftari la kumbukumbu la dhamana; na

(d) hisa za uanachama hazitumiki kama dhamana kwa mkopo unaotolewa na SACCOS.

Udhamini wa mkopo.

**35.-**(1) Mwanachama anaweza kudhamini mkopo wa mwanachama mwengine ikiwa anayedhamini ana dhamana za kutosha ikijumuisha hisa za hiari, akiba, amana za muda maalumu na dhamana nyengine zinazokubalika.

(2) SACCOS itamjulisha kikamilifu kila mdhamini juu ya dhima anayoibeba kabla ya kusaini mkataba wa dhamana.

(3) Endapo SACCOS imepokea malipo ya mkopo kutoka kwa mdhamini, SACCOS itatoa hati ya kuthibitisha kupokea malipo ya mkopo husika.

Miamala ya watu wanaohusiana.

**36.-**(1) SACCOS haitatoa mkopo kwa mjumbe wa Kamati ya Uongozi au kamati ya mikopo au watu wanaohusiana nao isipokuwa kama mkopo huo umeidhinishwa na wajumbe wengi wa Kamati ya Uongozi au kamati ya mikopo.

(2) Mjumbe wa Kamati ya Uongozi au kamati ya mikopo atatoka kwenye kikao ambacho maombi yake ya mkopo yanajadiliwa.

(3) SACCOS inaweza kumkopesha mfanyakazi wake kwa utaratibu maalumu utakaoidhinishwa na mkutano mkuu.

Urejeshaji wa mkopo kabla ya muda.

**37.-**(1) Mwanachama ana haki ya kurejesha mkopo kabla ya muda ikiwa wote au sehemu kwa kupunguza kiwango cha mkopo halisi, tozo na ada zinazodaiwa.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1) endapo mkopo utalipwa wote kabla ya muda wake, mwanachama hatatakiwa kulipa tozo kwa kipindi kilichosalia.

(3) SACCOS itaweka kumbukumbu sahihi za malipo yote ya mkopo kutoka kwa mkopaji zikionesha tarehe na kiasi kilichopokelewa.

Vigezo na masharti ya mikopo shirikishi.

**38.-**(1) SACCOS yenye leseni ya daraja A inaweza kukopa au kukopesha SACCOS nyengine kwa ajili ya kufidia upungufu wa ukwasi kwa masharti kwamba:

(a) SACCOS inayokopa haitazidi ukomo wa kukopa nje kama ilivyoelezwa katika Kanuni hizi;

(b) endapo kuna ombi la kukopesha au kukopa kwa SACCOS nyengine, itabidi kupata kwanza idhini ya mkutano mkuu;

(c) vigezo na masharti ya kukopa au kukopesha vitathibitishwa kwa makubaliano ya maandishi yaliyosainiwa kati ya SACCOS zinazoshiriki na makubaliano hayo yataidhinishwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa; na

(d) masharti ya kanuni ya 34 na 35 yatatumika sawa.

(2) Endapo SACCOS siyo mkopeshaji halisi, SACCOS hiyo itatakiwa:

(a) kushiriki katika mikopo inayoweza kuitoa tu;

(b) kuwa na sera ambayo imeweka viwango vya udhamini wa mikopo kabla ya kuingia kwenye makubaliano ya kushirikiana katika mikopo;

(c) kushiriki tu katika mikopo inayotolewa kwa wanachama wa SACCOS nyengine inayokopa;

(d) kubaki na mkataba halisi au nakala ya mkataba wa kushirikiana katika mikopo pamoja na jadweli la urejeshaji mkopo huo; na

(e) kupata idhini ya wajumbe wa Kamati ya Uongozi kwa ajili ya kutoa mkopo kwa mkopeshaji halisi.

Mikopo iliyochelele-weshwa kulipwa.

**39.-**(1) SACCOS itachukulia kuwa mkopo umecheleweshwa kulipwa endapo:

(a) malipo yaliyofanyika ni chini ya rejesho kamili lililopaswa kulipwa;

(b) mkupuo mmoja wa rejesho haujalipwa kuendana na masharti ya mkataba;

(c) mkopaji hajalipa rejesho kwa zaidi ya siku thelathini pale ambapo rejesho hilo ni riba au mkopo halisi; au

(d) ikiwa ni mkopo unaolipwa kwa mkupuo mmoja, jumla ya deni la msingi na riba havijalipwa ndani ya siku thelathini mara baada ya kupita kwa tarehe ya marejesho.

(2) Endapo mwanachama wa SACCOS ameshindwa kulipa mkopo wote au awamu moja ya marejesho mjumbe huyo hatapewa tena mkopo hadi atakapolipa deni lililopo.

Makundi na tengo la mikopo.

**40.-**(1) Kila SACCOS itagawa orodha ya mikopo yake kwenye makundi yafuatayo:

(a) iliyo ndani ya muda;

(b) angalizo;

(c) chini ya kiwango;

(d) mashaka na;

(e) hasara.

(2) Vigezo vya makundi ya mkopo na kiwango cha chini cha tengo

kwa kila kundi kitakuwa kama kilivyoainishwa katika Jadweli la Nne la Kanuni hizi.

(3) Kiwango cha chini cha tengo kwa kila kundi ni kama ifuatavyo:

Limbikizo la tozo kwa mikopo iliyocheleweshwa kulipwa.

**41.-**(1) SACCOS itasitisha limbikizo la tozo kwa mikopo iliyocheleweshwa kulipwa kwa zaidi ya siku tisini.

(2) Limbikizo lolote la riba au faida ambalo halijakusanywa chini ya kanuni ndogo ya (1) litawekwa kwenye akaunti ya dharura.

(3) SACCOS inaweza kurudisha mkopo kutoka katika hali isiyolimbikizwa na kwenda kwenye hali ya kulimbikizwa endapo mkopaji amelipa malimbikizo ya tozo na mkopo halisi.

Kukusanya au kufuatilia mikopo.

**42.-**(1) Kwa mujibu wa kifungu cha 52 cha Sheria, SACCOS itakusanya au kufuatilia mkopo kutoka kwa mkopaji kwa mujibu wa taratibu za makusanyo kama zilivyoainishwa kwenye sera ya mikopo.

(2) Kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba taratibu za kukusanya au kufuatilia mkopo zinazingatia misingi ya kumlinda mlaji, SACCOS:

(a) itatoa notisi ya maandishi ya siku kumi na nne kwa mkopaji kabla ya utaratibu wa kukusanya au kufuatilia deni haujaanza;

(b) haitamnyanyasa, kumdhalilisha au kumkandamiza mkopaji, mdhamini au mtu yeyote wakati wa ukusanyaji au ufuatiliaji wa deni;

(c) haitotisha au kutumia nguvu au njia isiyo halali katika kukusanya au kufuatilia deni;

(d) haitotumia lugha ya matusi au lugha isiyofaa;

(e) haitotumia maelezo au njia za uongo, udanganyifu au kupotosha au njia kama:

(i) kutoa taarifa ya uongo ya tabia ya mhusika, kiwango, kiasi, au hadhi ya kisheria ya deni lolote;

(ii) kutoa maelezo ya uongo kwamba mhusika ni wakili au mawasiliano yoyote yaliyofanywa yametoka kwa wakili;

(iii) kutishia kuchukua hatua yoyote ambayo haiwezi kuchukuliwa kisheria au kukusudiwa kuchukuliwa; au

(iv) kuwasiliana au kutishia kufanya mawasiliano kwa mtu yeyote kuhusu taarifa za mkopo ambazo zinajulikana kuwa ni za uongo.

(3) SACCOS haitakusanya riba, ada, tozo, au gharama isipokuwa kama zimeainishwa katika mkataba wa mkopo.

(4) SACCOS inaweza kumtumia mkusanya madeni kukusanya au

kufuatilia mkopo kutoka kwa mwanachama endapo mkusanya madeni huyo:

(a) ameidhinishwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa;

(b) anakusanya au kufuatilia madeni kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (2) na ya (3) ya kanuni hii; na

(c) anazingatia sheria husika zinazosimamia ukusanyaji wa madeni.

Ufutaji wa deni.

**43.-**(1) Kwa mujibu wa sera ya mikopo, SACCOS itafuta deni pale ambapo:

(a) mkopo upo kwenye kundi la hasara kwa zaidi ya mwaka mmoja;

(b) SACCOS imepoteza haki zake za kimkataba juu ya mkopo husika;

(c) imebainika kuwa mkopo hauwezi kulipika;

(d) hakuna matarajio ya marejesho ya mkopo kufuatia maamuzi ya mahakama dhidi ya mkataba wa ukopeshaji;

(e) dhamana zinazoshikiliwa zimefanyiwa tathmini na kuuzwa lakini mauzo yaliyopatikana hayatoshi kulipa deni lote; au

(f) SACCOS haina uwezo wa kukusanya mkopo na hakuna dhamana.

(2) Endapo mkopo umefutwa chini ya Kanuni hizi, SACCOS itahakikisha kuwa:

(a) taarifa za mkopo huo zinahifadhiwa nje ya mizania; na

(b) jitihada za ukusanyaji wa deni hilo zinaendelea.

## SEHEMU YA SITA
## USIMAMIZI WA UKWASI, MALI NA DHIMA

Sera ya usimamizi wa mali na dhima.

**44.-**(1) Kila SACCOS itaandaa sera ya usimamizi wa ukwasi, mali na dhima.

(2) Sera iliyotajwa katika kanuni ndogo ya (1) itajumuisha mambo yafuatayo:

(a) mtu atakayehusika kusimamia ukwasi, mali na dhima;

(b) Uwiano na njia zitakazotumika kusimamia ukwasi kama zilizowekwa katika Kanuni hizi;

(c) kiwango cha juu cha fedha taslimu kinachopaswa kuwepo;

(d) utaratibu wa mara kwa mara wa kuchambua hali ya

ukwasi, mali na dhima; na

(e) mpango wa dharura wa ukwasi.

(3) Sera iliyotajwa katika kanuni ndogo ya (1), itafanyiwa mapitio kila mwaka kuhakikisha kwamba inaendana na uhalisia.

(4) Sera ya usimamizi wa ukwasi, mali na dhima itawasilishwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa si zaidi ya siku thelathini baada ya kuwa imeidhinishwa na mkutano mkuu, na endapo kuna mabadiliko yoyote yamefanywa katika sera, SACCOS itaonyesha bayana maeneo yote yaliyoguswa na mabadiliko hayo.

Mpango wa dharura wa ukwasi.

**45.-**(1) SACCOS itaandaa na kuwasilisha Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa mpango wa dharura wa ukwasi ulioidhinishwa na mkutano mkuu kwa ajili ya kukabiliana na hali ya upungufu wa fedha.

(2) Mpango wa dharura wa ukwasi, kwa uchache utajumuisha taratibu za kurekebisha mapungufu ya fedha katika mzunguko, vyanzo vya fedha vinavyotegemewa, tathmini ya gharama za mikakati mbadala ya kupata fedha na athari zake katika mtaji wa SACCOS.

Kiwango cha chini cha uwiano wa ukwasi wa mali.

**46.-**(1) SACCOS itatakiwa kuwa na kiwango cha chini cha ukwasi wa mali kisichopungua asilimia kumi na tano ya akiba, amana, mikopo ya muda mfupi na madeni ya muda mfupi ya wanachama wake.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii, "ukwasi wa mali" unajumuisha:

(a) noti na sarafu ambazo ni fedha halali katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(b) amana zilizo katika benki na taasisi za fedha;

(c) dhamana za serikali za muda mfupi na muda mrefu ambazo hazina kizuizi, na

(d) mali nyengine yoyote ambazo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kuainisha.

Amana katika benki.

**47.** Isipokuwa kama imeruhusiwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, SACCOS haitaweka amana zinazozidi asilimia sitini ya mtaji halisi kwenye benki moja au taasisi za fedha.

Ukopaji nje ya SACCOS.

**48.-**(1) Baada ya kupata idhini ya mkutano mkuu, SACCOS inaweza kukopa kutoka vyanzo vya nje, kwa kuzingatia kuwa:

(a) mkopo huo umeidhinishwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa; na

(b) jumla ya mikopo yake ya nje haizidi asilimia hamsini ya jumla ya mali.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii, "ukopaji wa nje" maana yake

ni ukopaji kutoka kwa wasiyokuwa wanachama ikijumuisha benki na taasisi za fedha.

Sera ya uwekezaji.

**49.-**(1) Kila SACCOS itaandaa sera ya uwekezaji.

(2) Sera iliyotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) itajumuisha yafuatayo:

(a) uwekezaji unaoruhusiwa kwa mujibu wa sheria husika;

(b) ukomo wa uwekezaji kwa kila eneo la uwekezaji;

(c) utambuzi wa vihatarishi na mikakati ya kuvipunguza;

(d) aina na vipindi vya uwasilishaji wa taarifa Kamati ya Uongozi; na

(e) taratibu za uidhinishaji na ukomo wake.

(3) Sera iliyotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) itawasilishwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa si zaidi ya siku thelathini baada ya kuwa imeidhinishwa na mkutano mkuu, na endapo kuna mabadiliko yoyote yamefanywa katika sera, SACCOS itaonyesha bayana maeneo yote yaliyoguswa na mabadiliko hayo.

Masharti ya uwekezaji.

**50.-**(1) SACCOS haitafanya uwekezaji isipokuwa kama uwekezaji huo:

(a) unazingatia sera ya uwekezaji iliyoidhinishwa;

(b) unazingatia masharti ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Nam.15 ya 2018;

(c) umeidhinishwa na mkutano mkuu wa SACCOS; na

(d) ikiwa ni uwekezaji wa kifedha, uliofanywa kwa lengo la kuwekwa hadi kufikia kipindi cha muda wake.

(2) SACCOS inaweza kuwekeza katika:

(a) amana zilizo na riba kwenye benki au taasisi za fedha;

(b) dhamana za Serikali;

(c) SACCOS nyengine;

(d) mali zisizozalisha faida; au

(e) uwekezaji mwengine wowote kama itakavyoidhinishwa na Mkutano Mkuu.

(3) Endapo SACCOS itawekeza katika mali zisizozalisha faida, uwekezaji huo hautazidi:

(a) asilimia kumi ya jumla ya mali zake iwapo uwekezaji umefanyika kwenye mashine au vifaa; na

(b) asilimia tano ya jumla ya mali zake iwapo uwekezaji umefanyika kwenye ardhi na majengo, isipokuwa pale ambapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa imetoa ruhusa maalumu.

## SEHEMU YA SABA
## HESABU NA UKAGUZI

Vitabu vya hesabu na kumbu-kumbu.

**51.-**(1) SACCOS itatunza vitabu vya hesabu vilivyosahihi pamoja na kumbukumbu nyengine kuhusu shughuli zake ambazo zinaonyesha miamala na hali ya kifedha.

(2) Vitabu vya hesabu na kumbukumbu zilizotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1):

(a) vitaelezea kwa ufasaha miamala yote ikiwemo maombi na mikopo;

(b) zitaiwezesha hali ya kifedha ya SACCOS kujulikana kwa usahihi wakati wowote;

(c) zitawezesha uandaaji wa taarifa za fedha kwa wakati;

(d) zitajumuisha nyaraka za msingi ambazo zinahifadhiwa ili kuakisi taarifa za:

(i) jumla ya fedha zote zilizopokelewa na kutumika na masuala yanayohusu mapato na matumizi yaliyofanyika;

(ii) mauzo, manunuzi yote na miamala mengine; na

(iii) mali na madeni ya SACCOS.

Mwaka wa fedha.

**52.** Kwa madhumuni ya ufungaji wa hesabu, ukaguzi na utoaji wa taarifa, mwaka wa fedha wa SACCOS utaanza tarehe 1 Januari na kuishia 31 Disemba ya kila mwaka.

Uandaaji na uwasilishaji wa hesabu.

**53.** Kila SACCOS, katika kila mwaka wa fedha, itaandaa hesabu na ndani ya miezi minne kuanzia mwisho wa mwaka wa fedha kuwasilisha Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, hesabu za mwaka zilizokaguliwa na taarifa ya ukaguzi.

Uoneshaji wa taarifa za fedha.

**54.-**(1) Kwa mujibu wa kifungu cha 39 cha Sheria, kila SACCOS itaweka bayana katika sehemu yake ya biashara nakala ya taarifa zake za fedha zilizokaguliwa hivi karibuni.

(2) Taarifa za fedha zilizokaguliwa zinazotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1):

(a) zitajumuisha mizania, taarifa za mapato, taarifa za mtiririko wa fedha na taarifa za mabadiliko ya mtaji;

(b) zitawekwa eneo la wazi katika sehemu kuu ya biashara, matawi na vituo vya huduma; na

(c) zitawekwa kwa kipindi chote cha mwaka.

Mkaguzi wa ndani.

**55.-**(1) SACCOS itaajiri mkaguzi wa ndani katika kutathmini utoshelevu na ufanisi wa udhibiti wa ndani, udhibiti wa vihatarishi na mifumo ya utawala.

(2) Mkaguzi wa ndani aliyeajiriwa chini ya kanuni ndogo ya (1) atakuwa na, angalau, stashahada ya uhasibu au sifa inayofanana na hiyo na awe na uzoefu wa angalau mwaka mmoja katika fani husika.

(3) SACCOS inaweza kukodi huduma ya ukaguzi wa ndani kutoka kwa kampuni ya ukaguzi iliyosajiliwa au mtu binafsi mwenye sifa stahiki.

Taarifa ya mkaguzi wa ndani.

**56.-**(1) Mkaguzi wa ndani atawasilisha taarifa kwa Kamati ya Usimamizi.

(2) Taarifa za mkaguzi wa ndani zitakuwa na hoja za ukaguzi, mapendekezo na mrejesho kutoka Uongozi wa SACCOS.

Majukumu ya mkaguzi wa ndani.

**57.-**(1) Majukumu ya mkaguzi wa ndani yatajumuisha:

(a) kuhakiki fedha bila kutoa taarifa ya awali;

(b) kufanya ulinganisho wa akaunti za benki;

(c) kufanya ulinganisho baina ya salio la leja kuu na salio la leja ndogo;

(d) kukagua majalada ya mikopo kwa ajili ya kuangalia uzingatiwaji wa taratibu;

(e) uhakiki wa mali na uwekezaji wa SACCOS;

(f) kukagua utoshelevu wa tengo la hasara kwa mikopo isiyolipika;

(g) kukagua uzingatiaji wa sera na taratibu;

(h) kukagua uzingatiaji wa Sheria na sheria nyengine husika;

(i) kutathmini mwenendo na ukamilifu wa kumbukumbu za vikao na taarifa za utendaji;

(j) kutathmini utoshelevu wa mfumo wa usimamizi wa taarifa;

(k) kutathmini usahihi na kuaminika kwa taarifa za hesabu na taarifa za fedha;

(l) kubaini iwapo taarifa na maelezo yanayowasilishwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa ni sahihi na hutolewa kwa wakati;

(m) kubaini iwapo taratibu za uhasibu na mifumo ya udhibiti inatosheleza;

(n) kuhakiki utekelezaji na utunzaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani;

(o) kuhakikisha kuwa hoja na mapendekezo yote ya wakaguzi wa hesabu wa ndani na nje yanatekelezwa; na

(p) kutathmini ufanisi wa matumizi ya rasilimali.

Mpango wa ukaguzi wa ndani.

**58.-**(1) Mkaguzi wa ndani ataandaa mpango wa ukaguzi wa mwaka kwa ajili ya kazi atakazofanya katika mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Mpango wa ukaguzi uliotajwa katika kanuni ndogo ya (1) utajumuisha:

(a) muda na vipindi vilivyopangwa kwa kazi ya ukaguzi wa ndani;

(b) tathmini ya udhibiti wa ndani; na

(c) maelezo muhimu ya rasilimali watu na rasilimali nyengine;

(3) Mpango wa ukaguzi wa mwaka utawasilishwa kwa kamati ya usimamizi kwa ajili ya mapitio na kwa Kamati ya Uongozi kwa ajili ya kupata idhini kabla ya tarehe 31 Disemba kila mwaka.

Ukaguzi wa nje.

**59.-**(1) Hesabu za SACCOS zitakaguliwa angalau mara moja kwa mwaka na mkaguzi aliyesajiliwa ambaye ataidhinishwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

(2) Endapo SACCOS itashindwa kuteua mkaguzi wa nje wa hesabu au kujaza nafasi yeyote kwa ajili ya mkaguzi wa nje ambayo inaweza kujitokeza, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kuteua, kwa niaba ya SACCOS, mkaguzi wa nje na kupanga malipo yake ambayo yatalipwa na SACCOS.

(3) SACCOS haitakuwa bila mkaguzi wa nje kwa zaidi ya siku tisini kuanzia tarehe nafasi hiyo ilipokuwa wazi.

(4) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), mkaguzi wa nje hatafanya ukaguzi wa nje wa SACCOS kama mkaguzi huyo:

(a) ana uhusiano na maafisa au waajiriwa wa SACCOS; au

(b) ni mwanachama wa SACCOS husika.

Mkaguzi wa nje kuwasiliana na waajiriwa.

**60.** Mkaguzi wa nje anaweza kufanya mazungumzo na afisa wa SACCOS au afisa aliyekuwa ameajiriwa na SACCOS au mwajiriwa wa SACCOS kwa lengo la kupata taarifa muhimu kwa ajili ya ukaguzi husika.

Kutoa taarifa za ukiukwaji.

**61.** Mkaguzi wa nje atatakiwa kutoa taarifa kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa, ikiwa atagundua yafuatayo wakati anaendelea na ukaguzi:

(a) ukiukwaji mkubwa au kutokuzingatiwa kwa masharti ya Sheria, Sheria ya Kupambana na Utakasishaji wa Fedha Haramu na Mapato yatokanayo na Uhalifu, Nam.10 ya 2009 au Kanuni hizi;

(b) kosa lolote la jinai linalohusu udanganyifu au kutokuwa na uaminifu lililotendwa na SACCOS au viongozi wake au waajiriwa; na

(c) hasara zozote zilizopatikana ambazo zimesababisha SACCOS kuwa na upungufu wa mtaji.

Kuwasilisha taarifa za ukaguzi katika Mkutano Mkuu wa Mwaka.

**62.** Mkaguzi wa nje atawasilisha taarifa za ukaguzi katika Mkutano Mkuu wa Mwaka baada ya kupata ruhusa ya Kamati ya Uongozi.

Kubadilisha mkaguzi wa Nje.

**63.** SACCOS haitaruhusiwa, wakati zoezi la ukaguzi linaendelea, kumbadilisha mkaguzi wa nje isipokuwa pale itakapopata idhini ya maandishi kutoka Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

## SEHEMU YA NANE
## USIMAMIZI NA UKAGUZI

Ukaguzi wa SACCOS.

**64.-**(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa katika kutekeleza mamlaka yake ya ukaguzi chini ya Sheria, itafanya ukaguzi wa SACCOS kwa kupitia taarifa na nyaraka zilizowasilishwa kwake na zitakazopatikana kwa kuzuru ofisi ya SACCOS.

(2) Ukaguzi uliotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) utajumuisha yafuatayo:

(a) kuhakikisha SACCOS inatekeleza masharti ya kanuni na sera katika uendeshaji wa shughuli zake;

(b) kukagua uendeshaji na hali ya kifedha ya SACCOS;

(c) kutathimini ufanisi wa udhibiti uliopo dhidi ya uendeshaji, fedha na mali nyengine za SACCOS;

(d) kuchambua taarifa za mara kwa mara zinazowasilishwa na SACCOS; na

(e) masuala mengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

(3) Baada ya kukamilisha ukaguzi chini ya kanuni ndogo ya (1), Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kuandaa na kuwasilisha nakala ya taarifa ya ukaguzi kwa kamati ya uongozi au mkutano mkuu wa SACCOS.

(4) Kamati ya usimamizi wa SACCOS itahakikisha kwamba hatua stahiki zinachukuliwa kushughulikia hoja zilizobainishwa katika taarifa ya ukaguzi.

Uwasilishaji wa taarifa za vipindi.

**65.** SACCOS itawasilisha kwa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa taarifa za mara kwa mara kwa mfumo na vipindi vitakavyoanishwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

**66.-**(1) Endapo itabainika kwamba SACCOS haifanyi vizuri na taratibu za usimamizi za kawaida zimeshindwa kurekebisha hali iliyopo, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kuingia katika makubaliano ya pamoja ya usimamizi na kamati ya uongozi ya SACCOS ili kurekebisha mapungufu hayo. Makubaliano ya usimamizi.

(2) Makubaliano yaliyofanywa chini ya kanuni ndogo ya (1) yataweka hatua mahsusi za marekebisho au maboresho ndani ya muda ulioainishwa na yatasainiwa na kamati ya uongozi na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

(3) Endapo SACCOS itashindwa kutekeleza hatua zilizoainishwa ndani ya muda wa makubaliano ya usimamizi, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kufuta leseni yake.

**67.-**(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kutoa amri ya zuio na katazo kuielekeza SACCOS kushughulikia mienendo iliyo hatarishi au isiyofaa ambayo haijashughulikiwa ipasavyo kupitia hatua nyengine za usimamizi. Utoaji wa amri ya zuio na katazo.

(2) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kutoa amri ya zuio na katazo pale ambapo SACCOS:

(a) imejihusisha au inaendelea kujihusisha na mienendo yoyote ya kibiashara isiyo salama;

(b) imekiuka au inaendelea kukiuka Sheria, Kanuni hizi, kanuni au sera za SACCOS; au

(c) imeshindwa au inaendelea kushindwa kuzingatia makubaliano ya usimamizi.

**68.-**(1) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kuchukua usimamizi wa SACCOS endapo: Usimamizi na uchukuaji.

(a) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaona kuwa SACCOS husika:

(i) haipo katika hali nzuri ya kifedha;

(ii) haijiendeshi kwa mujibu wa misingi na taratibu stahiki za utawala na uhasibu;

(iii) haizingatii sera sahihi za udhibiti wa vihatarishi; au

(iv) haizingatii maelekezo yanayotolewa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

(b) SACCOS imeshindwa kuzingatia masharti ya kiwango cha chini cha mtaji kilichoainishwa katika Kanuni hizi;

(c) SACCOS imekataa kukaguliwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kama inavyotakiwa na Sheria;

(d) leseni ya SACCOS imefutwa; au

(e) SACCOS inaendesha biashara ya huduma ndogo za fedha kwa namna ambayo ni kinyume na Sheria au inaathiri maslahi ya wanachama.

(2) Baada ya kuchukua uendeshaji chini ya kanuni ndogo ya (1), Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kutumia huduma ya watu binafsi kusimamia SACCOS iwapo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itaona kwamba kufanya hivyo ndio njia sahihi, fanisi na ya gharama nafuu.

(3) Gharama za usimamizi wa SACCOS katika kipindi cha kuchukua usimamizi zitalipwa na SACCOS husika.

(4) Katika kipindi cha usimamizi hakuna mali yoyote ya SACCOS itakayoshikiliwa au kuhusishwa na dai la umiliki isipokuwa dai la umiliki lililowekwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

Ukomo wa usimamizi wa Benki au Mamlaka iliyokasi-miwa.

**69.-**(1) Usimamizi wa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa utasita endapo hali ya kifedha na kiuendeshaji ya SACCOS imeimarika au ndani ya miezi sita.

(2) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kuongeza kipindi cha miezi sita kilichotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) endapo hali ya kifedha na uendeshaji wa SACCOS haijaimarika.

(3) Mabadiliko yote yatakayofanywa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa katika sera, taratibu au usimamizi wa SACCOS katika kipindi cha usimamizi yatabaki kuwa halali hata baada ya kusita kwa usimamizi isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa.

(4) Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itatoa amri ya ufilisi kwa mujibu wa sheria endapo hali ya kifedha na shughuli za SACCOS hazijaimarika baada ya kuisha kwa miezi sita au muda wa nyongeza uliotolewa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa chini ya kanuni ndogo ya (2).

## SEHEMU YA TISA
## KUMLINDA MLAJI

Masharti ya uwazi wa hisa, akiba na amana.

**70.-**(1) Kila SACCOS itapaswa kuweka bayana kwa maandishi vigezo na masharti kuhusiana na kila hisa, akiba na amana za muda maalum kwa wanachama wake na wanachama tarajiwa.

(2) SACCOS itatoa taarifa za akaunti za hisa, akiba au amana kwa mwanachama anayeomba.

(3) Endapo akaunti itakuwa inamilikiwa na mwanachama zaidi ya mmoja au mkopo umetolewa kwa mwanachama zaidi ya mmoja, taarifa inaweza kutolewa kwa yeyote kati yao.

(4) Kwa akaunti zinazostahili gawio, SACCOS itaweka bayana viwango vya gawio vilivyopita au vinavyotarajiwa na asilimia ya mapato tarajiwa ya mwaka na njia iliyotumika kukokotoa gawio.

Mfumo wa utatuzi wa malalamiko na migogoro.

**71.-**(1) Kila SACCOS itakuwa na mfumo wa kushughulikia malalamiko na utatuzi wa migogoro ambao utajumuisha:

(a) namna ya kuwasilisha malalamiko;

(b) kuwepo na afisa maalumu ambaye atashughulikia malalamiko; na

(c) kipindi cha kushughulikia migogoro na kutoa mrejesho.

(2) Kila SACCOS itahakikisha kwamba mfumo wa kushughulikia malalamiko na utatuzi wa migogoro kwa wateja na taarifa za mawasiliano husika zinajumuisha namba za simu au barua pepe zimewekwa katika sehemu inayoonekana ya biashara, matawi na vituo vya huduma vilivyo wazi kwa umma.

(3) Taarifa zinazotajwa chini ya kanuni ndogo ya (2), zitakuwa katika lugha ya Kiswahili au lugha zote mbili, Kiswahili na Kiingereza.

Elimu ya fedha.

**72.-**(1) SACCOS itatoa elimu ya fedha kwa wanachama wake ambayo itajumuisha mambo yafuatayo:

(a) sifa muhimu za bidhaa na huduma zinazotolewa;

(b) vigezo na masharti ya mikopo;

(c) usimamizi wa mtiririko wa fedha;

(d) utunzaji wa kumbukumbu;

(e) maamuzi ya masuala ya fedha;

(f) usimamizi wa mikopo, matumizi na marejesho;

(g) mpango wa biashara;

(h) umuhimu wa kuweka akiba; na

(i) masuala mengine yoyote yanayoonekana ni muhimu.

(2) Elimu ya fedha iliyotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) inaweza kutolewa kupitia:

(a) vikao vya mtu mmoja mmoja;

(b) vipeperushi na vijarida;

(c) mafunzo;

(d) semina;

(e) kongamano;

(f) tovuti;

(g) vikao vya ushauri nasaha; na

(h) njia nyengine yoyote kama itakavyoonekana inafaa.

## SEHEMU YA KUMI
## MASHARTI MENGINEYO

Mpango wa mwendelezo wa biashara.

**73.-**(1) SACCOS itaandaa mpango wa mwendelezo wa biashara ambao utajumuisha yafuatayo:

(a) mtu au watu wenye wajibu wa kutekeleza, kufuatilia, kutathimini na kufanya mapitio ya mpango;

(b) wajibu na majukumu ya maafisa kufanya tathmini, kutoa taarifa na huduma kwa wanachama;

(c) utambuzi wa maeneo mbadala yenye vitendea kazi muhimu kwa ajili ya kusaidia shughuli muhimu kuendelea kufanywa kwa muda wa kutosha iwapo kutatokea majanga;

(d) utambuzi wa taarifa muhimu zinazohitajika kuendesha SACCOS kipindi cha majanga; na mpango wa usalama ulioandaliwa kwa ajili ya kulinda eneo la SACCOS.

(2) Mpango wa mwendelezo wa biashara utapitiwa na kujaribiwa angalau mara moja kwa mwaka.

Uwasilishaji wa taarifa za mikopo.

**74.-**(1) Baada ya SACCOS kupata utambulisho sahihi wa wakopaji itatoa taarifa kamili kwa taasisi za ubadilishanaji taarifa za mikopo kuhusu mikopo yote iliyotolewa kwa kila mkopaji kwa namna ambayo Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kuainisha.

(2) SACCOS itawasilisha kwa vyombo vya ubadilishanaji wa taarifa za mikopo kila mwezi taarifa za mikopo yote iliyotolewa na mipya.

(3) SACCOS itapata na kutumia taarifa za mikopo kutoka vyombo vya ubadilishanaji taarifa za mikopo kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Benki Kuu ya Tanzania (Taasisi za Ubadilishanaji wa Taarifa za Mikopo), 2012.

(4) SACCOS itatoa taarifa za mikopo sahihi na zinazojitosheleza kwa wakati.

(5) Bila kuathiri masharti ya kanuni hii, SACCOS itazingatia masharti ya Kanuni za Benki Kuu ya Tanzania (Taasisi za Ubadilishanaji wa Taarifa za Mikopo), 2012.

Ridhaa ya kubadilishana taarifa za mikopo.

**75.** SACCOS itahakikisha kwamba wakopaji wote wameridhia kwa maandishi kuiruhusu SACCOS kupata, kubadilishana au kuweka wazi taarifa zote za mikopo zinazohusu wakopaji, wakopeshaji au vyombo vya ubadilishanaji taarifa za mikopo.

Hatua za kiutawala.

**76.** Bila kuathiri adhabu na hatua zilizoainishwa chini ya Sheria, Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa inaweza kuchukua hatua zifuatazo za kiutawala dhidi ya SACCOS iliyokiuka masharti:

(a) zuio la kutangaza au kulipa gawio;

(b) zuio la kufungua au kuanzisha matawi au vituo vya huduma;

(c) kusitisha shughuli za ukopeshaji na uwekezaji;

(d) kufuta leseni;

(e) onyo rasmi kwa mjumbe wa kamati ya uongozi au meneja aliyekiuka taratibu;

(f) kumsimamisha mjumbe wa kamati ya uongozi au meneja;

(g) kumwondolea sifa ya kuendelea kushika cheo au nafasi yoyote katika SACCOS yoyote iliyo chini ya usimamizi wa Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa;

(h) adhabu ya kulipa kiasi cha fedha kitakachoamuliwa na Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa kisichopungua shilingi laki tano na kisichozidi shilingi milioni tano; na

(i) hatua nyingine zozote za kiutawala kama Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa itakavyoelekeza.

Rufaa.

**77.-**(1) Mtu ambaye haijaridhika na uamuzi ya Benki au Mamlaka Iliyokasimiwa chini ya Kanuni hizi anaweza kukata rufaa kwa Waziri, ndani ya siku thelathini, kutoka tarehe ya uamuzi.

(2) Rufaa chini ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii itakuwa kwa maandishi na itaeleza kwa uwazi:

(a) sababu za rufaa; na

(b) masuala mengine yoyote yanayohusika.

(3) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, Waziri ataamua rufaa ndani ya siku sitini kutoka tarehe ya kupokea rufaa.

(4) Katika kufanya uamuzi wa rufaa, Waziri anaweza kumtaka mkata rufaa kuwasilisha taarifa na nyaraka zote muhimu zinazounda msingi wa rufaa hiyo.

Kipindi cha mpito.

**78.-**(1) SACCOS ambayo ilikuwa ikifanya shughuli za huduma za fedha kabla ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi na ambayo inakusudia kuendelea kutoa huduma hiyo, ndani ya miezi kumi na mbili baada ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, itaomba Leseni kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi.

(2) SACCOS ambayo itashindwa kufuata masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, itafunga biashara na kuacha kutoa huduma.

Makubaliano kati ya SACCOS na waajiri.

**79.-**(1) Endapo SACCOS inakusudia kutoa huduma kwa wanachama ambao ni waajiriwa wa taasisi yoyote na ambao hisa, akiba, amana na malipo yao ya mikopo hufanyika kupitia makato ya mishahara, SACCOS husika itaingia makubaliano na mwajiri yatakayoainisha yafuatayo:

(a) vigezo na masharti kwa ajili vya kukusanya hisa, akiba na amana;

(b) masharti ya makato ya mkopo kutoka kwenye mshahara wa mwajiriwa na kuwasilisha kwa SACCOS;

(c) majukumu ya mwajiri na SACCOS; na

(d) masharti mengine yoyote husika.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii “huduma” inajumuisha ukusanyaji wa hisa, akiba, amana na utoaji wa mikopo.

**JADWELI LA KWANZA**

**FOMU YA MAOMBI YA LESENI**

**[Chini ya kanuni ya 4(1)]**

1. Jina la SACCOS: ……..................................………………….…………

   Namba ya Usajili: ……........……… Tarehe ya Usajili …………................

2. Mahali ilipo Ofisi Iliyosajiliwa: ……………………...…………………….

3. Anwani Halisi ya Makao Makuu: …………..….........……………………

   Namba ya Jengo …………………………………………………………

   Mtaa: ……………………..........................………………………………

   Shehia: ……………………....……………………………………………

4. Sanduku la Posta …………..…… Msimbo wa Posta ……..……..............…

   Namba ya Simu ...............................................................................................

   Barua pepe …………..…………………………………………………...

5. Endapo inafaa, majina ya maeneo ya biashara zilizopo Tanzania, mwaka zilipoanzishwa na miaka katika biashara.

| **Nam.** | **Jina la Tawi/Wakala/ Kituo cha Huduma** | **Mwaka ilipoanza** | **Idadi ya Miaka katika biashara** |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |

6. Endapo inafaa, orodha ya maeneo mengine ya biashara. Weka jina la mahali pa biashara, taja endapo ni huduma zinazohamishika; mashine ya kutolea fedha (ATM) au sehemu ya mauzo n.k.

7. Jina au majina ya awali, kama lipo/yapo, na ambalo/ambayo SACCOS ilijulikana kama:

   1. ......................................... kuanzia ......................... hadi ………………
   2. ......................................... kuanzia ......................... hadi ……...………

8. Maelezo ya Mtaji:

(a) Thamani iliyolipwa ….....…………..……………………………………

(b) Mtaji halisi ……………......….....…………………………………

(c) Mtaji taasisi …......…………..……………………………………....

9. Taarifa za Maafisa:

(a) Wajumbe wa Kamati ya Menejimenti

| Nam. | Jina Kamili | Anwani | Tarehe ya Uteuzi | Uzoefu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3 | | | | |

(b) Watendaji Waandamizi

| Nam. | Jina Kamili | Cheo | Sifa za taaluma/ utaalam | Mwaka ulipopata | Tarehe ya kuajiriwa | Ajira/ kazi ya awali |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | | |
| 2 | | | | | | |
| 3 | | | | | | |

10. Majina ya Benki na anwani zake

1. …………………...….....……… S.L.P ……………..……….......

2. ……………………...….....…… S.L.P ………………...….....…...

3. ……………………..…........… S.L.P …………………..…....…

11. Je SACCOS imewahi kuwekwa chini ya ufilisi au kuingia muafaka wowote au utaratibu na wadai wake au kushindwa kuwalipa wadai kikamilifu? .................. Kama ndivyo, toa maelezo …………………….....……........…
…………………………….............................……………………………..…
…………………………………………………………………………………

## JADWELI LA PILI

---

## MASHARTI YA LESENI

**[Chini ya kanuni ya 4(3)(a)]**

---

**Masharti kwa Leseni ya Daraja A**

(a) vipengele vyote vilivyoainishwa chini ya masharti kwa leseni ya Daraja B;

(b) mpango wa biashara wa miaka mitatu ya uendeshaji unaojumuisha:

  (i) Dira, Dhamira na Malengo;
  (ii) muundo wa Taasisi;
  (iii) bidhaa na huduma;
  (iv) mipango ya kuongeza matawi iwapo itahitajika;
  (v) mkakati wa ukuaji; na
  (vi) makisio ya mizania, mapato na matumizi na mtiririko wa fedha na vigezo vilivyotumika kufanya makisio kwa miaka mitatu ya uendeshaji; na

(c) sera za uwekezaji, rasilimali watu, akiba, ukwasi, fedha, makusanyo na miongozo ya taratibu na udhibiti wa ndani.

**Masharti kwa Leseni ya Daraja B**

(a) nakala ya sheria ndogo za SACCOS za wakati uliopo iliyothibitishwa;

(b) nakala ya cheti cha usajili kilichotolewa na Idara;

(c) majina kamili na anwani za wajumbe wa Kamati ya Uongozi, wajumbe wa Kamati ya Usimamizi na Maafisa waandamizi wa SACCOS;

(d) nakala ya sera ya mikopo;

(e) nakala ya kitambulisho cha Taifa, kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, kitambulisho cha mpiga kura, au Hati ya Kusafiria, kwa kila mjumbe wa Kamati ya Uongozi na Maafisa waandamizi;

(f) picha mbili za pasipoti kwa kila mjumbe wa Kamati ya Uongozi na maafisa waandamizi;

(g) azimio la mkutano mkuu kuhusu ridhaa ya kuomba leseni; na

(h) ushahidi wa malipo ya ada ya maombi.

**JADWELI LA TATU**

**[Chini ya kanuni ya 6(3)]**

**BENKI YA TANZANIA/MAMLAKA ILIYOKASIMIWA**

LESENI NAM. MSP3-

**LESENI YA KUENDESHA BIASHARA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA**

Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Zanzibar, Nam. 9 ya Mwaka 2023

**DARAJA ………..**

LESENI hii imetolewa kwa ......................................................................... (Jina la SACCOS) Nam. ya Usajili …………………….……ya ............................... (Anwani) na inaidhinisha SACCOS husika kuendesha biashara ya huduma ndogo za fedha Zanzibar chini ya Daraja la 3 katika Daraja……………………..…….. la Leseni.

Leseni hii imetolewa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Nam 9 ya Mwaka 2023 na masharti yaliyoainishwa katika barua yetu yenye Kumbukumbu Nam. ………...............................… ya tarehe ……….......………

Imetolewa leo …………...................……… tarehe ……………………………

**JINA NA SAINI**

## JADWELI LA NNE

## MAKUNDI NA TENGO LA MIKOPO

**[Chini ya kanuni ya 40(2)]**

### A. VIGEZO VYA MAKUNDI YA MKOPO

| Idadi ya siku zilizocheleweshwa | Kundi |
|---|---|
| Siku 0 hadi 30 | Iliyo ndani ya muda |
| Siku 31 hadi 90 | Angalizo |
| Siku 91 hadi 180 | Chini ya kiwango |
| Siku 181hadi 365 | Mashaka |
| Zaidi ya siku 365 | Hasara |

### B. KIWANGO CHA CHINI CHA TENGO KWA KILA KUNDI

| Kundi | Tengo |
|---|---|
| Angalizo | 10% |
| Chini ya Kiwango | 30% |
| Mashaka | 50% |
| Hasara | 100% |

**ZIMETIWA SAINI** leo tarehe 20 Mei, 2025

**(DKT. SAADA MKUYA SALUM)**
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO**
**ZANZIBAR**

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR-2025